



Athletics
Integrity
Unit

Power Of Respect



Maelezo kuhusu
Whereabouts

Mahali ulipo ni nini?

Taarifa kuhusu mahali ulipo hutumiwa na Athletics Integrity Unit (AIU) kuwapata wanariadha kwa ajili ya vipimo vya nje ya mashindano bila taarifa ya mapema, ambayo ni muhimu sana katika Mpango wa Vipimo wa AIU.



RTP ni nini?

World Athletics Registered Testing Pool (RTP) ni kundi teule la wanariadha bora ambao hupimwa mara kwa mara nje ya mashindano na wanawajibika kutoa ujumbe kuhusu mahali walipo.



Kuwa mwanariadha wa RTP kunamaanisha



Wewe ni miongoni mwa wanariadha bora duniani, ni mafanikio makubwa!



Unaheshimu mchezo wako na hadhi yako kama kielelezo.




Unataka kulinda sifa yako, na ya mchezo wetu, na taifa lako tukufu.



Unachangia katika kuunda uwanja wa ushindani sawa katika riadha, kwa kupeana ujumbe wa mahali ulipo.

Ujumbe zinazohitajika

- Mahali pa kulala usiku
- Muda wa dakika 60 unayopatikana
- Ratiba ya mashindano
- Shughuli za kawaida (ikiwa ni pamoja na ratiba ya mazoezi na kazi/masomo ikiwa inafaa)
- Ratiba ya Kusafiri





Kumbuka

Unatakiwa kutoa maelezo ya kina ya kutosha kuhusu mahali ulipo ili kumwezesha DCO kukupata kwa ajili ya vipimo visivyotarajiwa, bila kupiga simu au kuwauliza majirani maelekezo. AIU kwa kawaida huwaonya DCOs wasipige simu.

Unaweza kupimwa wakati wowote, hata nje ya muda wako wa dakika 60..

AIU, NADO yako na NADO nyingine zenye mamlaka zinaweza kutumia taarifa kuhusu mahali ulipo kukupima..

Eleza AIU ikiwa uko mjamzito, umejeruhiwa au unataka kustaafu.

Huwezi kukataa kupimwa.
Kukataa = kupimwa kuwa na hatia, hivyo uwezekano mkubwa wa kufungiwa kwa miaka 4. Mara tu unapogundua DCO yuko hapo ili kukupima, lazima uatii..



Love

Respect

Protect

Mazoezi Bora

✈️ Jumuisha mashindano na safari mara tu usajili au nafasi inahakikishwa.

🕒 Weka kengele kabla ya muda wako wa dakika 60 na ukae mahali ulipoonyesha kwa muda wote wa dakika 60.


🛏️ Jumuisha nambari ya chumba wakati unakaa kwenye hoteli na ujumilishe dawati kuhusu haja yako ya kupatikana kwa ajili ya vipimo.

📝 Jumuisha maelezo ya ziada, picha, au uratibu wa GPS inapohitajika

Muda wa kuwasilisha taarifa kuhusu mahali ulipo

Taarifa kuhusu mahali ulipo lazima iwasilishwe mara nne kwa mwaka na lazima isasishwe mwaka mzima. Tarehe za mwisho za robo mwaka ni **Machi 15, Juni 15, Septemba 15, na Desemba 15.**

Baada ya kuwasilisha, lazima usasishe taarifa kuhusu mahali ulipo mara tu unapojua mabadiliko katika hali yako.



Njia za kuwasilisha ujumbe kuhusu mahali ulipo


DAMS Website ama Athlete Central App. Kama Athlete Central App iko chini na unafaa kupeana ujumbe wa mahali ulipo tuma ujumbe kwa barua pepe whereabouts@athleticsintegrity.org.



Tazama mafunzo yetu ya video

ADAMS tutorial – [Youtube](#)

Athlete Central tutorial – [Youtube](#)



Download on
App Store



Download on
Google Play

Kuna aina mbili za kushindwa kutoa taarifa kuhusu mahali ulipo



Vipimo Vilivyokosekana

Haupatikani kupimwa wakati wa muda wa dakika 60



Kushindwa Kuwasilisha Maelezo ya mahali ulipo

Taarifa kuhusu mahali ulipo zisizokamilika au zisizo sahihi, kuwasilishwa kwa kuchelewa, na visasisho vya dakika za mwisho visivyo na sababu.

Madhara yanayoweza kutokea kwa kutotumiza jukumu ya kufuata masharti ya kupeana ujumbe wa mahali ulipo

- Kufungiwa na michezo ambayo inaweza kudumu hadi miaka miwili
- Kufutiliwa kwa matokeo
- Hasara ya kifedha
- Athari mbaya kwa hadhi yako ya kijamii, sifa na uwezo wa kupata sponsors.

Wakilishi

Kama mwanariadha wa RTP, una jukumu la kuhakikisha kuwa taarifa zako za mahali pa ulipo ziko sawa na zimesasishwa kila wakati. Unaweza kumpa mtu mwingine jukumu hilo, kama vile kocha, meneja, au mwanachama wa familia, ili ajulishe taarifa zako za mahali ulipo kwa niaba yako. Lakini unahitaji kudumisha mawasiliano mazuri kati yako na mtu huyo ili kuhakikisha usahihi wa taarifa zako za mahali ulipo. Wanafaa kujua vizuri matokeo ambayo utakabiliana nayo kwa makosa yoyote. Kumbuka, wewe ndiye una jukumu la mwisho kwa kushindwa kufuata mahitaji ya kupeana ujumbe wa mahali ulipo.

Kumbuka, wewe ndiye una jukumu la mwisho kwa kushindwa kufuata mahitaji ya kupeana ujumbe wa mahali ulipo.

Maswali ama unahitaji maelezo ya ziada?



Uliza [ADAMS Help Centre](#).



Tuma barua pepe kwa whereabouts@athleticsintegrity.org



Tuma mahitaji ya mafunzo kwa education@athleticsintegrity.org

 aiu_athletics

 aiu_athletics

 aiu.athletics

